



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

MASUALA YA KUZINGATIA BAADA YA KUFUNGWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

Dar es Salaam, 19 Oktoba, 2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wote wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Pili ya udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2020/2021 imefungwa rasmi tarehe **18 Oktoba, 2020**. Zoezi linaloendelea ni vyuo kuchakata na kuidhinisha maombi ya udahili yaliyopokelewa vyuoni katika Awamu ya Pili ya udahili. Zoezi la kuchakata na kuidhinisha maombi hayo litakapokamilika, majina ya waliodahiliwa katika awamu ya pili yatatangazwa na vyuo husika tarehe **24 Oktoba, 2020**.

Aidha, muda wa kuthibitisha udahili kwa waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza ya udahili umemalizika tarehe **17 Oktoba, 2020**. ***Waombaji ambao bado hawajakamilisha uthibitisho wao, watapewa utaratibu mwingine wa kujithibitisha na hakuna mwombaji atakayekosa udahili kwa sababu ya kushindwa kujithibitisha.***

Tume inawaasa waombaji wote ambao hawajaweza kutuma maombi ya udahili katika Awamu ya Kwanza na ya Pili kutokana na sababu mbalimbali, wawe na subira na watapewa maelekezo mahususi ya kuzingatia.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa

KATIBU MTENDAJI

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA